JINA LA MTEJA	NAMBARI YA ACES ID

Haki na Majukumu Yako Unapopokea Huduma Zinazotolewa na Idara ya Maisha ya Nyumbani na Jamii na Idara ya Ulemavu wa Ukuaji

Your Rights and Responsibilities When You Receive Services Offered by Home and Community Living Administration and Developmental Disabilities Administration

Huduma Zilizopo

Una haki ya kuchagua kutoka kwenye huduma ambazo unastahili kupokea. Huduma hizi ni za kujitolea. Huduma ambazo Idara ya Maisha ya Nyumba na Jamii na Idara ya Ulemavu wa Ukuaji zinaweza kulipia huenda zisikusaidie mahitaji yako yote.

HCLA na DDA wanatoa huduma katika:

- Nyumba ya Wazee, Kituo cha Kuishi Kinachofadhiliwa, Kituo cha Huduma Zilizoboreshwa, Kituo cha Huduma za Uuguzi, ICF/IDs, Nyumba ya Mwenza, Nyumba ya Malezi ya Watoto, Nyumba ya Makazi ya Watoto Inayohudumiwa na Wafanyakazi wenye Leseni; Nyumba za Pamoja za DDA, Nyumba za Mafunzo ya Pamoja, AU
- Nyumba binafsi ya mhusika. **Kumbuka:** HCLA na DDA hawatoi huduma zilizolipiwa za uangalizi binafsi kwa muda wa saa 24 katika nyumba binafsi ya mhusika. Ikiwa huduma ya saa 24 itahitajika, basi chaguzi za huduma nyingine zinaweza kufikiriwa.

Wakala wa Eneo Lako wa Kesi za Uzee, Meneja wa Rasilimali za Kesi za DDA, Mshauri wa Huduma kwa Wauguzi, Mshauri wa Utunzaji, Mtaalamu wa Huduma za Kijamii za Nyumbani na Jamii, au Meneja wa Kesi za Kituo cha Wauguzi cha HCS anaitwa **mfanyakazi anaeshughulika kesi** katika hati hii.

Haki Zako

Una haki ya:

- Kushughulikiwa kwa utu, heshima na bila ubaguzi;
- Kuhakikisha mali yako inaheshimiwa;
- Kufanya kazi kwa kushirikiana na anayeshughulikia suala lako katika kupanga huduma zako za uangalizi;
- Unaweza kuomba huduma ya ukalimani bila gharama yoyote kama huwezi kuzungumza au kuelewa Kiingereza vizuri;
- Kufanya taarifa zako kuwa za siri ndani ya mipaka ya sheria na kanuni za DSHS;
- Kutolazimishwa kujibu maswali au kufanya kitu usichokitaka;
- Kuambiwa kuhusu huduma zote unazoweza kupata na kufanya maamuzi kuhusu huduma unazozitaka au usizozitaka;
- Kutaarifiwa kwa maandishi juu ya maamuzi ya shirika husika na kupata nakala ya mpango wako wa uangalizi au muhtasari wa mpango wa usaidizi;
- Kataa huduma zote;
- Chagua, futa kazi, au badilisha mtoa huduma anaefaa; na
- Pokea matokeo ya utafiti wa historia ya mtoa huduma yeyote binafsi uliyemchagua;
- Kuongea na msimamizi wako iwapo wewe na anayeshughulikia suala yako hamkubaliani katika jambo fulani;
- Wasilisha malalamiko au wasiwasi wakati wowote kuhusu utendaji wa jimbo au wa mtoa huduma kuhusu mchakato wako wa kupanga utunzaji, mpango wa utunzaji, huduma, au kitu chochote ambacho hujaridhika nacho nyumbani kwako na katika mazingira ya kijamii. Una haki ya kuwasilisha malalamiko bila kulipiza kisasi. Unaweza kuwasilisha malalamiko au wasiwasi kwa kupiga simu 1-800-737-0617, kutuma barua pepe kwa grievances@dshs.wa.gov, au kumuuliza mfanyakazi yeyote wa DDA au HCLA taarifa kuhusu jinsi ya kuwasilisha malalamiko;
- Kuomba haki na usawa mbele ya utawala (administrative hearing) hata kama umeshatoa malalamiko;
- Toa malalamiko bila kuogopa hata kama umeomba haki na usawa mbele ya utawala (administrative hearing);
- Zungumza na mwanasheria kwa kupiga 1-888-201-1014; na
- Usinyanyaswe, usipuuzwe, kunyonywa kifedha, au kutelekezwa. Kwa maelezo ya masharti haya, tembelea: https://www.dshs.wa.gov/altsa/home-and-community-services/types-and-signs-abuse. Ikiwa wewe au mtu unayemjua anatendewa vibaya, anapuuzwa au ananyanyaswa, tafadhali piga simu ya bure ya DSHS kwa 1-866 (End Harm) /1-866-363-4276 ili kuzungumza na mfanyakazi ambaye anaweza kukusaidia.

Barcode label

16172

JINA LA MTEJA	NAMBARI YA ACES ID

Majukumu Yako

Una wajibu wa:

- Kumruhusu anayeshughulikia kesi yako afanye tathimini yako angalau kila mwaka katika eneo lenye maslahi kwako;
- Kumruhusu anayeshughulikia kesi yako achunguze mazingira unayoishi angalau kila mwaka;
- Kutupa taarifa za kutosha ili tukamilishe tathmini yako na kusaidia katika uratibu wa mpango wako wa utunzaji;
- Kumtaarifu anayeshughulikia suala lako iwapo mtu mwingine ndiye anayefanya maamuzi ya kitabibu au kifedha kwa niaba yako;
- Kushiriki katika uandaaji wa mpango wako wa uangalizi au wa usaidizi, na utie saini;
- Kujibu na kuwasiliana na mfanyakazi anaeshughulia kesi yako kwa wakati unaofaa;
- Kuchagua huduma yako binafsi ya matibabu;
- Kuchagua mtoa huduma mwenye vigezo;
- Kuhakikisha utafiti wa historia linakuwa jambo binafsi;
- Kuelewa kwamba mtoa huduma wako hawezi kulipwa kwa huduma au saa ambazo hazijaidhinishwa;
- Kumweleza mfanyakazi anaeshughulikia kesi yako kama una matatizo na mtoa huduma wako au hupewi huduma kwa saa zinazotozwa na mtoa huduma wako;
- Kumlipa mtoa huduma wako kila mwezi kama unachangia kulipia huduma za uangalizi wako;
- Kutoa mahali salama pa kazi;
- Kutotenda kwa namna ambayo inamweka mtu yeyote hatarini;
- Kumwambia mfanyakazi anaeshughulikia kesi yako kabla ya kuondoka, ikiwa unasafiri nje ya jimbo la Washington na mtoa huduma wako binafsi; na
- Kumtaarifu mfanyakazi anayeshughulikia kesi yako kama kuna mabadiliko katika:
  - ✓ Hali yako ya kiafya;
  - ✓ Msaada unaopata kutoka kwa familia, marafiki, au mashirika mengine;
  - ✓ Hali yako ya kifedha;
  - ✓ Mahali unapopokea huduma yako;
  - ✓ Mahali unapoishi katika jimbo la Washington; au
  - ✓ Makazi yako - kupanga kuhama, au kwa sasa unaishi nje ya jimbo la Washington.

Wajibu wa Anayeshughulikia Suala lako

Anayeshughulikia suala lako anawajibika:

- Kukushughulikia kwa utu na heshima;
- Kudumisha usiri wako;
- Kukwambia nini HCLA na DDA wanaweza, au hawawezi, kukufanyia;
- Kupata taarifa kutoka kwako na watu wengine ili kufanya tathimini itakayoamua ngazi yako ya usaidizi na itakayoamua ni huduma gani unaweza kuzichagua;
  - ✓ Tathimini hio itajumuisha uwezo wako, udhaifu wako, malengo yako na mapendeleo yako;
  - ✓ Tathimini hii itajumuisha msaada ambao tayari unaupata au unaoweza kuupata kutoka kwa familia au mashirika mengine na namna unavyotaka huduma hizo kufanywa;
- Kukusaidia kuandaa mpango wa uangalizi au mpango wa usaidizi unaoshughulikia usaidizi wa huduma binafsi ya uangalizi na inajumuisha malengo yako binafsi, mapendeleo binafsi na chaguo binafsi;
- Kupata taarifa kutoka kwako na watu wengine ili kuboresha mpango wako wa uangalizi au mpango wako wa usaidizi kila mwaka au pale hali yako inapobadilika;
- Kukupatia muda wa kutosha kuandaa taarifa zinazohitajika;
- Kushughulikia matatizo ya mpango wako wa uangalizi au wa usaidizi pale yanapojitokeza;
- Kuheshimu haki zako na kutoa msaada zaidi wa kuhudumiwa kama una ulemavu wa akili, ulemavu wa neva, hisia, au ulemavu wa mwili; na
- Kukusaidia kutafuta mtoa huduma mwenye vigezo kama hutaweza kumpata yeyote.

Barcode label

16172

JINA LA MTEJA	NAMBARI YA ACES ID

Maelekezo ya Awali

Una haki ya kutoa maelekezo ya awali. Maelekezo ya awali huweza kujumuisha wosia wa mtu ambaye bado anaishi au nguvu thabiti ya mwanasheria kwa ajili ya huduma yako ya afya. Maelekezo ya awali yanatoa muhtasari wa shauku zako kuhusu mpango wa uangalizi wa afya ya akili, ikiwa ni pamoja na haki ya kukubali au kukataa matibabu ya dawa, akili, afya au upasuaji, kama huna uwezo wa kiakili wa kufanya maamuzi hayo. Unaweza kubatilisha maelekezo yako ya awali wakati wowote.

Huduma ya Usajili wa Mpiga Kura

Sheria ya Taifa ya Usajili wa Mpiga Kura ya 1993 inahitaji majimbo yote kutoa usaidizi wa usajili wa mpiga kura kupitia ofisi zao za msaada kwa umma. Kujisajili au kukataa kujisajili kupiga kura hakutaarithiri huduma au kiwango cha mafao utakayopatiwa na shirika hili. Kama ungependa msaada wa kujaza fomu ya usajili wa mpiga kura, tutakusaidia. Uamuzi wako wa kujisajili au kukataa kujisajili utafanywa kuwa siri na kutumika tu kwa ajili ya madhumuni ya usajili wa mpiga kura. Ikiwa unaamini kwamba kuna mtu ameingilia haki yako ya kujisajili au kutojisajili kupiga kura, haki yako ya usiri katika kuamua ama kujisajili au kutuma maombi ya kujisajili kupiga kura, au haki yako ya kuchagua chama chako binafsi au mapendeleo mengine ya kisiasa, unaweza kuwasilisha malalamiko na:

Washington State Elections Office
PO Box 40229
Olympia WA 98504-0229
1-800-448-4881

Saini Yako

Tia saini hapo chini ikiwa unaelewa haki na wajibu wako na unaelewa wajibu wa anayeshughulikia suala lako.

Saini ya Mteja	Tarehe
Saini ya Mwakilishi wa Kisheria	Tarehe

Ilani kwa wateja na waajiriwa (Title VI na VII) Idara ya Jimbo la Washington ya Huduma za Jamii na Afya ni mwajiri anayezingatia fursa sawa na habagui katika eneo lolote la uajiri, programu zake au huduma zake kwa misingi ya umri, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, jinsia, utambulisho wa jinsia, hali ya ndoa, mbari, imani, rangi, asili ya utaifa, asili ya dini au imani, msimamo wa kisiasa, hali ya kijeshi, mwanajeshi mstaafu aliyemaliza muda wake kwa heshima, uwepo wa ulemavu wowote wa neva, akili au mwili au matumizi ya mbwa-mwongozi aliyepewa mafunzo au huduma ya wanyama kwa mtu mwenye ulemavu, malipo sawa au taarifa za vinasaba.

Barcode label

16172

Haki na Majukumu Yako Unapopokea Huduma Zinazotolewa na Idara ya Maisha ya Nyumbani na Jamii na Idara ya Ulemavu wa Ukuaji

Maagizo ya Mfanyakazi Anaeshughulia Kesi

1. Pitia fomu hio na mteja ili kujibu maswali yoyote kuhusu haki na majukumu ya mteja. Pitia na mteja katika tathmini ya awali ya CARE (au katika Mabadiliko Muhimu/Mwaka ikiwa fomu hio haijasainiwa). Ikiwa kuna toleo lililosasishwa la fomu, mwambie mteja asaini fomu hio iliyosasishwa. Fomu ya hivi karibuni ya haki na majukumu ya mteja iliyowasilishwa na mfanyakazi anaeshughulikia kesi na kusainiwa na mteja inachukua nafasi ya fomu zilizosainiwa awali.
2. Mwambie mteja au mwakilishi wa mteja atie saini nakala mbili za fomu hio kuonyesha uelewa wake wa haki na majukumu ya mteja wakati wa kupokea huduma zinazotolewa na Idara ya Nyumba na Jamii na Idara ya Ulemavu wa Ukuaji.
3. Weka nakala moja katika rekodi ya kesi ya mteja ya kielektroniki na mpe mteja nakala nyingine.